# HAKI ZA MWANAMKE

## KWA MUJIBU WA QUR'AN NA SUNNAH ZA MTUME (S.A.W)

## TOLEO JEPESI

KONRAD ADENAUER STIFTUNG

# Haki za Mwanamke

## kwa Mujibu wa

# Qur'an na Sunna

**Toleo Jepesi**


**Zanzibar Female Lawyers Association**
**(ZAFELA)**

Kimetayarishwan na:
Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA)
S.L.P. Zanzibar
zafelamember@yahoo.com
+255 777 003 347

Utayarishaji na uchapaji wa kitabu hiki umefadhiliwa na:
Konrad-Adenauer- Stiftung (KAS)
S.L.P 6992
Mtaa wa Ismani, Upanga
Dar es Salaam, Tanzania
+255 22 2153174
www.kas.de/tanzania

Kimesanifiwa na
yasin.yusuph@yahoo.co.uk

ISBN: 978-9976-5674-5-8

© ZAFELA / Konrad-Adenauer-Stiftung, 2020

Sehemu yoyote ya kitabu hiki inaweza kunakiliwa na kubadilishwa kukidhi mahitaji yanayotakiwa bila kuomba idhini ili mradi machapisho yote yatolewe bure. Machapisho yoyote ambayo ni kwa ajili ya biashara yatahitaji kibali kutoka ZAFELA/KAS.

ZAFELA/KAS watashukuru kupatiwa nakala ya chapisho lolote ambalo sehemu ya maandishi yake yamenukuliwa kutoka kitabu hiki.

Angalizo: Mawazo yaliyomo katika kitabu hiki yanatokana na ZAFELA wenyewe wala si msimamo wa Taasisi ya KAS.

# Yaliyomo

Utangulizi ........................................................................................... iv

1. Mwanamke Kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) .......................... 1

2. Haki ya Mwanamke katika Elimu ................................................... 3

3. Haki ya Mwanamke katika Uongozi na Ushirikishwaji .................... 5

4. Haki ya Mwanamke katika Uchumi na Ajira ................................... 8

5. Haki ya Mwanamke katika Ndoa .....................................................11

6. Haki ya Mwanamke katika Mirathi .................................................13

7. Nafasi ya ZAFELA katika Kupigania Haki za Wanawake ..................15

# Utangulizi

**Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu (S.W)** aliyeteremsha kwa waja wake Kitabu na Sheria ili awatoe katika giza la ujinga na kuwaingiza katika nuru na ustaarabu. Sala na Salamu zimshukie Mtume Muhammad (S.A.W) aliyetumwa ili awe rehma kwa walimwengu wote, pamoja na jamaa zake na wote waliomfatia mpaka siku ya kiama. Ama baada ya hayo.

Kitabu hiki cha **HAKI ZA MWANAMKE KWA MUJIBU WA QUR'AN NA SUNNA ZA MTUME (S.A.W)** kimekusanya na kuyaweka pamoja mengi ya maelezo yaliyotawanyika katika Sura nyingi za Qur'an Tukufu na vitabu mbalimbali vya Hadithi. Kazi hii imeleta nafuu na kuwa msaada muhimu kwa wale wasio na uwezo au ujuzi wa kutambua au kudadavua upeo wa mambo moja kwa moja kutoka katika Qur'an Tukufu na vitabu vengine vya Sunna.

Kutokana na maombi yaliyopelekwa ZAFELA, kitabu hicho kimefanyiwa ufupisho kwa kutolewa kwa njia ya maswali na majibu ili iwe rahisi zaidi kumkumbusha aliye mjuzi, wepesi kwa anayejifunza huelewa juu ya hoja mbalimbali na hata kumsaidia mwanafunzi kuhifadhi na kufahamu ushahidi, ufafanuzi na majibu ya shubuha (mambo yenye kutatanisha).

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kitabu hiki kiwe na manufaa makubwa na azidishe jitihada za waliokitayarisha katika mizani ya mema yao siku ya mwisho.

# Mwanamke Kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W)

**Swali:** **Je, mwanamke alikuwa na hali gani kabla ya kuja Mtume Muhammad (s.a.w)?**

**Jibu:** Kabla ya kuja Mtume Muhammad (s.a.w), mwanamke alikuwa akiishi katika madhila makubwa;

- Alionekana kama bidhaa tena ambayo haina thamani;
- Alikuwa haruhusiwi kumiliki chochote;
- Hakuwa na haki ya kurithi, bali yeye mwenyewe aliweza kurithiwa;
- Hakuwa anapewa nafasi yeyote ya uongozi (cheo);
- Alionekana kama mtu wa kutia aibu familia yake na ndio akawa anaozeshwa mapema kukimbiza aibu kwa jamaa zake;
- Mwanamme alioa wanawake bila idadi maalum na kuwaacha bila ya idadi ya talaka nk.

**Swali:** **Je, tabia hii ilijengeka kutokana na mafunzo ya Vitabu na Mitume iliyotangulia?**

**Jibu:** Hapana, tabia hii haikuamriwa wala kuletwa na Mwenyezi Mungu (S.W), bali ni tabia ambayo ilijengeka miongoni mwa wanadamu wenyewe na kuanza kufanya unyanyasaji, ubaguzi na ukandamizaji wa kijinsia na waliyoongoza kuyafanya hayo ni wanaume na mifumo isiyojuzu mafunzo ya Allah.

**Swali:** **Je, kuna ushahidi wowote wa Qur'an au Sunna za Mtume Muhammad (s.a.w) unaoonesha Uislamu haumbagui mwanamke?**

**Jibu:** Qur'an Tukufu imeweka bayana juu ya usawa kati ya mwanamke na mwanamme kupitia Sura mbalimbali; mfano **Aya 97 ya Surat An-Nahl** inasema:

﴿مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ۝٩٧﴾ [النحل: 97]


**Tafsiri**

**"Na watakaofanya vitendo vizuri, wakiwa wanaume au wanawake hali wao ni wenye kuamini, basi hao wataingia peponi wala hawatadhulumiwa hata ugamba wa kokwa ya tende."** *(Surat An-Nahl 16:97).*

Kwa ushahidi huo wa maneno ya Mwenyezi Mungu; inabainisha kwamba mwanamme na mwanamke wote ni sawa katika majukumu na haki.

Aidha kwa lengo la kutilia mkazo ushahidi huu, hadithi ya Mtume (s.a.w) inasema:

**"Wanawake ni ndugu baba mmoja, mama mmoja na wanamume, wanayo haki kwa sheria (kufanyiwa na wanamume) kama ile haki iliyo juu yao kuwafanyia wanamume"** *(Abu Dawoud).*



# Haki ya Mwanamke katika Elimu

Baada ya kuja Mtume Muhammad (s.a.w) na kushushwa kwa Qur'an Tukufu, Uislam ulileta mtazamo mpya uliotofautiana na mitazamo ile iliyotangulia juu ya nafasi ya mwanamke katika kupata elimu. Uislam ulikuja kumkomboa mwanamke katika masuala ya elimu kwa kuondosha mtazamo kuwa; haki na wajibu wa kutafuta elimu ni kwa wanaadamu wote bila ya kujali jinsia.

**Swali:** **Je, Uislam unamruhusu mwanamke kupata elimu?**

**Jibu:** Ndio, Uislam haujambagua mwanamke katika jukumu la kutafuta elimu. Wakati Mwenyezi Mungu (S.W) alipoteremsha Qur'an alimsisitiza mwanadamu kutafuta elimu, kuelimisha na kuifundisha bila ya kuweka mipaka baina ya mwanamke na mwanamme. Wote wawili walitakiwa kutii amri ya kutafuta elimu.

**Swali:** **Je, kuna ushahidi wowote wa kutilia mkazo jibu hilo?**

**Jibu:** Ndio, kuna ushahidi wa Aya na Sunna/ Hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w).

Qur'an inathibitisha ukweli huo katika **Sura ya 96 (Al-alaq), Aya 1:**

اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِى خَلَقَ

**Tafsir: "Soma kwa jina la Mola wako aliyekuumba."**

Aidha, kupitia aya ya 5 ya sura hiyo hiyo ya 96, Mwenyezi Mungu anasisitiza kuwa amemfundisha mwanadamu mambo aliyokuwa hayajui. Bila ya kutaja jinsia ya kike au ya kiume.

عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ

**Tafsir: "Amemfundisha mtu aliyokuwa hayajui"**

Kadhalika, Mtume Muhammad (s.a.w) amesema kwenye Hadithi maarufu kuwa:

**"Kutafuta elimu ni faradh (lazima) kwa Muislamu Mwanamke na mwanamme"** *(Imepokelewa na Bukhary na Tabaraniy).*

Pia katika Hadithi nyengine, Mtume Muhammad (s.a.w) amesema: **"Anayeulizwa kuhusu taaluma akaificha, ataungwa kamba za moto siku ya Kiama"** *(Imepokelewa na Ahmad, Abuu Daud, Nasi, Tirmidhy na Ibnu Majad).*

**Swali:** **Je, kuna mfano wowote wa wanawake wanachuoni katika zama za mwazoni mwa Uislamu?**

**Jibu:** Naam, wapo wanawake wengi waliokuwa wanachuoni tokea zama za masahaba na katika karne nyengine za mwanzo. Mfano wa wanawake hao ni Bibi Aisha mke wa Mtume Muhammad (s.a.w), bibi Suhaila binti Al-Husein – Nafisatul Ilmu na Rabiat Al-Adamiyy.

# Haki ya Mwanamke katika Uongozi na Ushirikishwaji



**Swali:** **Je, nini maana ya uongozi?**

**Jibu:** Uongozi ni mamlaka au karama ya kuonesha watu njia kwa vitendo kufikia kwenye lengo lililokusudiwa. Qur'an Tukufu imedhihirisha wazi kuwa jukumu la kuendesha jamii lipo kwa wote; wanawake na wanaume. Qur'an inawataka wote washirikiane katika kuamrisha mema na kukataza mabaya na yale yote yanayovuruga Amani.

**Swali:** **Je, uislamu umeweka misingi ipi katika uongozi na ushirikishwaji hususan kwa mwanamke?**

**Jibu:** Uislamu umeweka misingi imara katika suala zima la uongozi na ushirikishwaji bila ubaguzi baina ya mwanamke na mwanamme.

Kigezo kikubwa kilichowekwa ni uwezo wa mtu na uchamungu wake. Ingawa suala hili bado lina mzozo mkubwa baina ya Maulamaa lakini Qur'an haijakataza mwanamke kuwa kiongozi.

**Swali: Je, kuna uthibitisho wa Aya na Hadithi hizo?**

**Jibu:** Naam, **Surat- ul Al-Namli, Aya ya 15–42** imelezea kwa upana sifa za kiongozi ikijumuisha zifuatazo;

- Mwenye elimu, hekima na busara.
- Mwenye kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwathamini wenzake na wote anaowaongoza.
- Aliyeandaliwa vyema kiuongozi ili aweze kuendeleza mazuri atakapofikia. Aidha mwenye uwezo wa kuandaa viongozi watakaoendeleza atakapofikia.
- Aliye muadilifu na mwenye kusimamia uadilifu na haki.
- Mwenye uwezo wa kutafuta, kupanga na kudhibiti rasilimali na nyenzo kwa nidhamu na uwezo wa hali ya juu.
- Mwenye uwezo wa kusikia vilio na kero za watu wa chini na uthubutu wa kuitikia kwa haraka.
- Asiye na kiburi kwa kukiri kutokamilika kwake hivyo kuwa tayari kukosolewa, kushauriwa na kuelekezwa.
- Awe ni mwenye kuthamini na kukiri juhudi na fadhila za waliomtangulia.
- Mwenye uwezo wa kufuatilia watendaji wa kada tofauti na uthubutu wa kuwawajibisha kwa mujibu wa utendaji wao.
- Msamehevu na mwenye kuchunga hali, dharura na mazingira yanavyokwenda.
- Mwenye kuhakiki taarifa anazopelekewa na kuzifanyia kazi.
- Mwenye dira, mikakati hai na anayejiamini katika kutoa maamuzi.
- Aliye tayari kupambana na rushwa katika hali zote.

Aidha Mtume Muhammad (s.w) amesema: **"Nyote ni wachunga na kila mmoja ataulizwa kwa alichokichunga"**

**Swali:** **Je, mwanamke anaweza kuwa kiongozi?**

**Jibu:** Kutokana na sifa zilizotajwa hapo juu mwanamke hajakatazwa kuwa kiongozi. Uislam umesititiza kuwa kila mtu ni mchunga na ataulizwa kwa alichokichunga. Hii inamaanisha kwamba kila mtu ana jukumu la kusimamia, kushauri na kuongoza na ikiwa hatafanya hivyo basi Mwenyezi Mungu atakuja kumuuliza kwanini hakutekeleza majukumu yake kama alivyoamrishwa.

﴿وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ
الْمُنْكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۚ أُولَٰئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ
اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾﴾ [التوبة: 71]

**Tafsiri:**
**"Na waumini wanaume na waumini wanawake wao kwa wao ni wasimamizi huamrisha mema na hukataza maovu"** *(Sura ul A-Tawbah (9:71).*

**Swali:** **Je, kuna mfano wowote wa wanawake wanachuoni katika zama za mwanzoni mwa Uislamu?**

**Jibu:** Naam, wapo wanawake wengi ambao walikuwa ni wanachuoni tokea zama za masahaba na katika karne nyengine za mwanzo. Mfano wa wanawake hao ni Bibi Aisha mke wa Mtume (s.a.w) bibi Suhaila binti Al-Husein – Nafisatul Ilmu na Rabiat Al-Adamiyy.



# Haki ya Mwanamke katika Uchumi na Ajira



**Swali:** **Je, mwanamke wa Kiislamu anaruhusiwa kufanya shughuli za kiuchumi zitakazo muingizia kipato hata kama yupo kwenye ndoa?**

**Jibu:** Mwanamke wa kiislamu anaruhusiwa kujishughulisha na uchumi na kupata kipato chake cha halali. Mwanamke kama ilivyo kwa mwanamme pia anatakiwa kutoa Zaka, Sadaka, kwenda Hijja, kusaidia ndugu na jamaa na pia kuchangia njia mbalimbali za Mwenyezi Mungu. Jambo la msingi la kuzingatia ni kujiheshimu na kujihifadhi na kufuata maadili ya Dini.

**Swali:** **Ipo kauli inayoeleza kuwa mwanamke ni pambo la nyumbani. Je, atawezaje kufanya kazi kwa kujiajiri au kuajiriwa? Si atakuwa anapingana na Sheria za Kiislamu?**

**Jibu:** Mwenyezi Mungu (S.W) alisisitiza watu kufanya kazi hakubagua ni jinsia ipi wafanye na wengine wasifanye. Katika **Sura ya 62 (Surat-ul Al- Jumu'a), Aya ya 10,** Mwenyezi Mungu (S.W) anasema:

﴿فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانْتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا مِنْ فَضْلِ اللَّهِ وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٠﴾﴾ [الجمعة: 10]

**Tafsir**

**"Na itakapokwisha swala, tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi, (ili msipate kufanya mabaya), ili mpate kufaulu"** *(Surat-ul Al- Jumu'a, 62:10).*

Pia katika **Sura ya 4 (Suratul An-nisaa)**, Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَامًا وَارْزُقُوهُمْ فِيهَا وَاكْسُوهُمْ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَعْرُوفًا ﴿٥﴾﴾ [النساء: 5]

**Tafsir**

**"Wala msiwape wapumbavu mamlaka ya kuzitunza mali zenu ambazo Mwenyezi Mungu amezifanya kuwa ndiyo njia yenu ya kujikimu, wale ambao hawana uwezo kiakili wa kumiliki mali. Kwa hiyo walisheni na wavisheni vizuri tu na zungumzeni nao kwa upole."** *(Suratul An-nisaa, 4:5).*

Kupitia Aya hizo Mwenyezi Mungu amewaamrisha wanaadamu wote kufanya kazi kwa lengo la kujipatia kipato cha halali ili kujikimu kimaisha. Hivyo, si sahihi kusema mwanamke ni pambo la nyumba na asifanye kazi, ukizingatia mwanamke naye ana wajibu wa kutoa Zaka, Sadaka, kusaidia mayatima, kwenda Hija n.k. kama ilivyo kwa mwanamme.

Pamoja na kuruhusiwa kufanya kazi, lazima kazi hizo ziwe za halali na zifanywe kwa njia ya stara na heshima.

Aidha, ipo Hadithi sahihi ya Mtume Muhammad (s.a.w) inayosisitiza umuhimu wa kila mtu kufanya kazi: **"Mmoja wenu kuchukua kamba akenda kufunga kuni ni bora kuliko kuomba omba..."**



**Swali:** **Je, upo mfano wowote wa wanawake ambao walikuwa wakifanya kazi?**

**Jibu:** Ndio, wapo wanawake waliokuwa wanamilikiki uchumi mkubwa na kuwasaidia waislamu wengine, miongoni mwa watu hao ni Bibi Khadija Binti Khuwaled.

# Haki ya Mwanamke katika Ndoa




**Swali:** **Nini maana ya ndoa na ni ipi nafasi ya mwanamke katika ndoa?**

**Jibu**: Ndoa ni mapatano ya kisheria kati ya mwanamme na mwanamke. Ni mkataba wa hiyari unaofungwa na mafungamano baina ya mke na mume kwa kuwepo mashahidi na walii wa mwanamke. Lengo kuu la ndoa ni kuishi kwa upendo, huruma, maelewano na amani. Ili ndoa ifungwe ni lazima ipatikane ridhaa ya mwanamke na apewe mahari.

**Swali:** **Ni zipi haki na majukumu ya mwanamke katika ndoa kwa mujibu wa mafundisho ya Qur'an na Sunna?**

- **Haki ya kuchagua mume**; si kama wanavyodhania watu wengi kuwa mtoto wa kike ni mtu wa kuchaguliwa mume tena kwa nguvu hata kama mume hamtaki. (hadithi ya binti aliyeozeshwa).

- **Haki ya kushauriwa**; mwanamke ana haki ya kushauriwa na kutoa maoni yake kabla ya kufunga ndoa na ndani ya maisha ya ndoa, kuzaa na kunyonyesha. (Hii kutokana na hadithi ya Abuu Huraira (R.A)).

- **Haki ya kupewa mahari**; kwa lengo la kuonesha upendo na kumthamini mwanamke. Kisheria, mahari ni haki ya anayeolewa (mwanamke) na si ya wazazi wake. (Suratul Nisaa).

- **Haki ya matunzo**; uislamu umempa mume jukumu la kumtuza mke wake kwa kumkamilishia mahitaji yake yote kama vile chakula, mavazi, malazi na tendo la ndoa; sambamba na kumsimamia katika mambo yake yote hata kama mwanamke ana uwezo kumpita mume wake. Labda tu pale mwanamke atakapojikubalisha kumsaidia mume wake lakini halazimiki kufanya hivyo. (Suratul Nisaa).

- **Haki ya kutendewa wema;** mwanamme ana wajibu wa kumtendea wema mke wake kwa kila hali, pia ni wajibu wa mwanamme kumsomesha mke wake kama mwanamke huyo elimu yake ni ndogo. Wema huu unatakiwa ufanyike hata baada ya kuvunjika kwa ndoa. Mwanamke anatakiwa abakie kwenye nyumba ya mume wake hadi amalize eda yake na pia apewe kitoka nyumba.

- **Haki ya kuvunja ndoa;** inapotokea ulazima wa kuvunja ndoa na mwanamme hayupo tayari kutoa talaka basi mwanamke kapewa nafasi hiyo kwa mujibu wa Sheria za Dini ya Kiislamu. Sheria imempa mwanamke nafasi ya kujivua ndoa (Khuluu) pale ambapo amechukizwa na mwanamme (bila ya sababu ya msingi) na kuhofia kutokutekeleza haki za ndoa basi mwanamke atalazimika kurejesha mahari (Hadithi ya Thabit Qays).

# Haki ya Mwanamke katika Mirathi




**Swali:** **Kwanini Uislamu unaonekana unamnyima mwanamke wa kiislamu mirathi?**

**Jibu.** Hapana, kauli hiyo si sahihi kabisa. Kabla ya kuja Mtume Muhammad (s.a.w) mwanamke alikuwa hapewi kitu chochote katika mirathi, kwa hoja ya kwamba yeye hapigani vita wala halindi nchi. Waarabu walikuwa na msemo wao “Tutampaje mali mtu ambaye hapandi farasi, hachukui upanga wala hapigani na adui?” Baada ya kuja Mtume Muhammad (s.a.w) na kushuka Aya za mafungu ya mirathi, bado baadhi ya watu walikataa kwa kusema “….tumpe mwanamke robo ya mali au thumni na tumpe mtoto wa kike nusu na apewe mtoto mdogo mwanamme na hali ya kuwa hapana kati yao anayepigana na maadui na apewe ngawira?” (Amepokelewa na Ibn Jariir kutoka kwa Ibni Abass (R.A)).

Uislam unamjali sana mwanamke na umempa mirathi kwa mafungu tofauti kulingana na nafasi yake kwa anayemrithi.

Kuna baadhi ya wakati mwanamke na mwanammme wanarithi sawa mfano anapokufa mtu akawaacha watoto wake wa kike na kiume pamoja na wazazi wake wote wawili, hapa wazazi kila mmoja atapata sudusi 1/8 ya mali ya marehemu (Surat-ul An-nisaa, Aya ya 11,12 na 176).

# Nafasi ya ZAFELA katika Kupigania Haki za Wanawake



Mwanamke ni hazina muhimu katika maisha ya binadamu, bila ya mwanamke ulimwengu ungebaki na upweke usiomithilika. Sambamba katika maisha yetu ya kila siku, mwanamke ni mtu muhimu sana na anastahiki kutunzwa kwa kupatiwa haki zake sawa na mwanamme ili naye aishi katika maisha ya utu na heshima.

Jumuiya ya wanasheria wanawake Zanzibar (ZAFELA), imekuwa ikifanya jithada mbalimbali kuhakikisha kuwa utu wa mwanamke unathaminika kwa kupatiwa haki zake stahiki. Katika kutimiza hilo, ZAFELA inashirikiana na washirika mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, ikiwemo shirika la **KAS** ambao ni washirika wakuu katika kutayarisha kitabu cha HAKI ZA MWANAMKE KWA MUJIBU WA QUR'AN NA SUNNA ZA MTUME (S.A.W) pamoja na toleo hili ambalo limeandaliwa katika mfumo wa maswali na majibu.

**Swali: Je, ni jinsi gani ZAFELA wanaweza kumsadia mwanamke kudai haki?**

**Jibu:** Mwanamke yeyote mwenye uhitaji wa msaada wa kisheria na ushauri kuhusu haki zake anaweza kufika katika ofisi za ZAFELA zilizopo Mchina Mwanzo njia ya Jang'ombe, mkabala na mnara wa zantel.

**Swali: Je, ni haki zipi hasa zinaweza kudaiwa kupitia ZAFELA?**

**Jibu:** Haki za aina zote ambazo mwanamke anastahiki lakini amekoseshwa basi anaweza kufika kwenye ofisi za ZAFELA kusaidiwa. Uvunjwaji wa haki umegawika katika sehemu kuu mbili. Kuna haki ambazo aina ya kesi huwa za madai. Kesi za aina hiyo huwa zinasimamiwa na ZAFELA moja kwa moja kwa kufanya usuluhishi au kutayarisha hati za madai na kuzipeleka mahakamani. Aidha, kuna haki nyingine zenye sura ya jinai ambazo ZAFELA huzisimamia kwa kufanya ufatiliaji na kuhakikisha Mamlaka husika zinatoa haki stahiki kwa walalamikaji.

**Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA)**
**S.L.P. Zanzibar**
**zafelamember@yahoo.com**
**+255 777 003 347**

Kabla ya kuenea kwa Uislamu, historia imemwelezea mwanamke kama kiumbe dhalili aliyekuwa hapewi haki wala nafasi katika jamii. Mwanamke aliishi kwa kudharaulika, kunyanyaswa na kuteswa akionekana kama mkosi katika familia, hali hiyo ilipelekea watoto wa kike kuuawa kwa kuzikwa wakiwa hai.

Baada ya mwanamke kuishi katika dhulma hiyo kwa muda mrefu, bila ya kupata haki zake, Allah (S.W) alimtuma Mtume wake (S.A.W) kuja kumkomboa mwanamke ili aondoke katika dhulma na udhalilifu aliokuwa akiupata kutoka kwenye jamii anayoishi.

Suala la nafasi ya mwanamke katika Uislamu ni moja kati ya mabadiliko makubwa yaliyokuja kumkomboa mwanadamu dhidi ya ujahilia (ujinga). Hata hivyo kumekuwa na shutma nyingi zinazopotosha usahihi wa jambo hili. Hii inatokana na ukosefu wa uelewa sahihi, lakini pia kutokana na tabia mbaya ya baadhi ya watu ambao huchanganya mafundisho ya Uislam na matamanio yao.

Kitabu hiki kinaelezea haki za mwanamke kwa mfumo wa maswali na majibu ili kumsaidia msomaji kuelewa haki hizo kama zilivyotajwa katika Qur'an na Sunnah kwa kumwelezea mwanamke kama kiumbe mtukufu, mwenye huruma na anayestahiki haki zote za kibinadamu.

**ISBN 978-9976-5674-5-8**